



CHUO KIKUU CHA KUMBUKUMBU YA ABDULRAHMAN AL-SUMAIT - ZANZIBAR

(CHUO KIKUU CHA SUMAIT)

Chuo Kikuu cha Kumbu Kumbu ya Abdulrahman Al-Sumait kinatangaza nafasi za masomo ya mafunzo ya Lugha ya Kiarabu kwa muda wa miezi minne.

SIFA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO.

Mafunzo hayo yatakuwa wazi kwa muombaji yeyote na hatalazimika kuwa na sifa za juu za kitaalamu ili aweze kujiunga. Madhumuni makuu ya mafunzo hayo ni kuboresha uelewa na ufahamu wa kuzungumza na kuandika Lugha ya Kiarabu.

MAFUNZO YATAKAVYOTOLEWA.

Mafunzo ya Lugha ya Kiarabu yatasomeshwa na wahadhiri maalum waliobobea na wenye uzoefu mkubwa katika idara ya Lugha ya Kiarabu ya Chuo Kikuu cha SUMAIT.

MADA NA UTOAJI MAFUNZO.

Mafunzo yatatolewa kwa siku za Jumatatu, Jumanne na Jumamosi kuanzia saa 8:00 mchana hadi saa 12:30 jioni, zikiwemo dakika 30 za mapumziko ya sala ya Alaasir.

GHARAMA ZA MAFUNZO.

- a) Fomu za maombi 5000/=
- b) Ada ya Usajili 30,000/=
- c) Ada ya ufundishaji 300,000/=
- d) Ada ya mitihani 30,000/=

NAMNA YA KUJIUNGA NA MAFUNZO.

Fomu za maombi zinapatikana katika Afisi ya Kitengo cha Elimu Endelevu (Continuing Education Unit) Chuo Kikuu cha SUMAIT Chukwani Zanzibara au kwenye tovuti ya Chuo www.sumait.ac.tz

Gharama za fomu ya maombi, usajili, utoaji wa mafunzo na mitihani zote zitalipwa kwa kutumia nambari ya Banki ya watu wa Zanzibar, (kitengo cha Banki ya Kiislamu) Akaunti Na: 51120100002450 Mwanakwerekwe au Mpirani Madema Zanzibar.

Fomu za maombi zitazojazwa pamoja na risiti za malipo zinatakiwa kurejeshwa katika Afisi ya Wahasibu wa Chuo Chukwani kabla ya tarehe 21/4/2017.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Mkuu wa Kitengo cha Elimu Endelevu

Chuo Kikuu cha SUMAIT

S.L.P 1933 ZANZIBAR

Nambari za Simu za mkononi 0777-426-913 au 0772-332-225

AU

Fika Chuo Kikuu cha SUMAIT kiliopo Chukwani, Wilaya ya Magharibi B, kiasi cha kilomita mbili kutoka jengo jipya la Baraza la Wawakilishi Zanzibar.